JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**OFISI YA WAZIRI MKUU**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

# MAHUSIANO BAINA YA MADIWANI NA WATUMISHI WA HALMASHAURI

Dodoma
**Januari, 2006**

# MAHUSIANO BAINA YA MADIWANI NA WATUMISHI WA HALMASHAURI

## UTANGULIZI

1. Serikali za Mitaa ni vyombo vya wananchi vilivyoanzishwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria za Serikali za Mitaa kutekeleza majukumu yafuatayo:

   (a) Kutekeleza kazi za Serikali za Mitaa ambazo ni pamoja na kutoa huduma za msingi kwa wananchi kama zilivyoainishwa katika sheria mbalimbali;
   (b) Kuhakikisha utekelezaji wa sheria na ulinzi wa wananchi; na
   (c) Kuimarisha demokrasia na kuitumia demokrasia hiyo kuharakisha maendeleo ya wananchi.

   Ili kutekeleza majukumu hayo, Halmashauri za Wilaya na za Miji ambazo huundwa na wajumbe wanaowakilisha wananchi (Madiwani) zimepewa uwezo wa kuajiri na kuwasimamia watumishi wa namna na fani mbalimbali ambao ndio hufikisha huduma mbalimbali kwa wananchi.

## 2. MISINGI YA JUMLA YA UONGOZI WA KISIASA NA UTENDAJI KATIKA HALMASHAURI

### Jukumu la Msingi la Diwani

Diwani huchaguliwa na wananchi ili kuwawakilisha kwenye vikao vya Halmashauri na kutafsiri shauku na mahitaji ya wananchi katika maamuzi yanayofikiwa kwenye mikutano ya Halmashauri na Kamati za Halmashauri. Jukumu la msingi la Diwani ni kushirikiana na Madiwani wenzake, na watumishi wa Halmashauri na umma kwa ujumla, katika kuhakikisha kuwa maamuzi muhimu yanayohusu utekelezaji wa shughuli za Halmashauri yanafanywa na yanatekelezwa kwa mujibu wa sheria kwa ajili ya ustawi na maendeleo ya wananchi kwenye eneo la Halmashauri husika.

### Majukumu ya Kisiasa ya Madiwani

Kwa kifupi, Majukumu makuu ya kisiasa ya Madiwani ni kama ifuatavyo:

(i) Kutunga sera na kuweka malengo na vipaumbele vya mipango na shughuli za Halmashauri;
(ii) Kufanya mashauriano na wananchi ili kujua matakwa na matarajio yao, kuhusu mipango ya maendeleo na upatikanaji wa mapato n.k.;
(iii) Kusimamia utekelezaji wa sera za Halmashauri kwa kuidhinisha na kufuatilia utekelezaji wa mipango na bajeti ya Halmashauri;
(iv) Kusimamia watumishi wa Halmashauri kwa kupitia menejimenti na kamati inayoshughulika na masuala ya utumishi ili kuhakikisha kuwa watumishi wanawajibika na kutimiza matakwa ya wananchi; na
(v) Kutoa maamuzi kwa masuala yanayoletwa kujadiliwa katika vikao na kutoa maagizo kwa watendaji.

Jukumu hili la kusimamia watumishi wa Halmashauri na kutoa maagizo limekuwa likileta mahusiano mabaya katika baadhi ya Halmashauri kutokana na baadhi ya wajumbe wa Halmashauri kutoa amri au maagizo kinyume na taratibu za kawaida za utawala.

Kwa mujibu wa Kanuni za Maadili ya Madiwani za mwaka 2000 maamuzi yote, maelekezo, amri na miongozo inayotolewa na Halmashauri ili kutekeleza majukumu yake, hupaswa kutolewa katika mikutano yake au ya Kamati za Halmashauri zilizokasimiwa uwezo wa kufanya maamuzi kwa niaba ya Halmashauri kulingana na taratibu zilizoelekezwa katika Kanuni za Kudumu za Halmashauri.

Diwani haruhusiwi kabisa kuingilia katika utendaji au uongozi wa idara yoyote ya Halmashauri. Hii ni pamoja na:

- Kutoa au kujaribu kutoa maelekezo, amri au miongozo kwa mtumishi yeyote au wakala wa Halmashauri;

- Kumzuia au kujaribu kumzuia mtumishi au wakala wa Halmashauri kutekeleza maamuzi ya Halmashauri au ya kamati ya Halmashauri;

- Kushawishi au kushiriki katika tendo lolote litakalosababisha au kuchangia katika uongozi mbaya ndani ya Halmashauri.

Kwa kifupi kanuni muhimu ya kuzingatiwa na Madiwani pamoja na viongozi wa kisiasa katika Serikali za Mitaa ni kutojiingiza katika shughuli za utendaji na kutoa maagizo kwa watumishi nje ya utaratibu wa kutumia vikao husika kwa mujibu wa sheria.

## Jukumu la Msingi la Watumishi wa Halmashauri

Jukumu la msingi la mtumishi wa Halmashauri ni:

- Kutekeleza kazi alizopangiwa kwa mujibu wa masharti ya ajira yake;
- Kutoa ushauri wa kitaalamu na kitaaluma kwa Halmashauri inayomwajiri;
- Kutekeleza maagizo ya mwajiri (Halmashauri) kwa uaminifu, uangalifu na ufanisi wa kiwango cha juu;
- Kutekeleza sera za Halmashauri pamoja na mipango na maamuzi yake, na kuwasaidia Madiwani kitaalamu na kiufundi katika kutekeleza majukumu yao ya uwakilishi na utoaji wa maamuzi.

## Majukumu ya Timu ya Menejimenti (Watumishi Wakuu)

Majukumu ya watumishi kwa jumla ni mengi sana lakini kwa kuwa watumishi wanaokuwa katika uhusiano wa mara kwa mara na Madiwani ni Mkurugenzi wa Halmashauri na Wakuu wa Idara ambao kwa pamoja huitwa Timu ya Menejimenti, majukumu ya Timu ya Menejimenti ni kama yafuatavyo:

- Kutoa ushauri sahihi na wa kitaalamu kwa Madiwani;
- Kuwezesha Madiwani kutoa maamuzi yanayozingatia sheria na miongozo iliyopo;

- Kutoa taarifa za mara kwa mara za ukusanyaji na matumizi ya fedha na utekelezaji wa mipango na shughuli za Halmashauri;
- Kutekeleza maagizo au maamuzi ya Halmashauri/Kamati za Halmashauri bila kukawia na kwa utiifu na uaminifu wa kiwango cha juu hata kama hawakubaliani nayo;
- Kuunganisha na kuwasilisha kwenye mikutano ya Halmashauri na Kamati za Halmashauri rasimu ya mipango na bajeti ya Halmashauri ili kujadiliwa na kuamuliwa kwa mujibu wa sheria na Kanuni za Fedha za Halmashauri;
- Kutekeleza bajeti na mipango ya kazi;
- Kuimarisha na kuendeleza ujuzi wa watumishi;
- Kuimarisha mwenendo mzuri wa uendeshaji wa siku hadi siku wa kazi, kama vile utoaji huduma au shughuli za fedha na makusanyo ya mapato; na
- Kutekeleza majukumu yao kwa uwazi na kuwajibika ipasavyo kwa Halmashauri na kwa umma kwa ujumla.

Ni muhimu wajumbe wa Halmashauri kufahamu kuwa si kila agizo watakalolitoa linaweza kutekelezwa na watumishi. Ingawa kimsingi ni jukumu la watumishi kutekeleza maagizo ya Halmashauri, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa ya 1982 (Kifungu 63) inalifanya kosa la jinai kwa mtu yeyote, awe Diwani au mtumishi wa Halmashauri, kufanya kitendo chochote chenye lengo la kuhatarisha fedha za Halmashauri au kushiriki katika kitendo au shughuli yoyote yenye lengo la kuzuia utozaji au ukusanyaji wa kodi au mapato mengine ya Halmashauri. Kwa hiyo, Madiwani wakitoa maagizo ambayo ni kinyume na sheria (na ambayo kusema kweli ni kinyume na uwezo iliopewa Halmashauri) ni dhahiri kuwa watumishi hawatakubali kutenda kosa la jinai kwa kuyatekeleza maagizo ya aina hiyo.

## Majukumu ya Watumishi wa Ngazi za chini

Majukumu ya watumishi wa kawaida ambao si Wakuu wa Idara, ni kama yafuatayo:

- Kutoa na kufikisha huduma kwa wananchi;
- Kufanya shughuli za kifedha na kutunza vitabu vya hesabu kulingana na bajeti na mipango ya kazi;

- Kuweka kumbukumbu za matumizi ya rasilimali na kufuatilia mipango ya kazi;
- Kufanya kazi za siku hadi siku na kutekeleza taratibu nyingine zozote wanazopangiwa na wakuu wao wa kazi; na
- kutoa taarifa za mara kwa mara kwa wakuu wao wa kazi kama taratibu za utendaji kazi wao zinavyoelekeza.

**Msimamo wa Sheria Juu ya Mahusiano Baina ya Madiwani na Watumishi**

Uzoefu unaonesha kwamba migogoro mingi ya mahusiano baina ya Madiwani na watumishi (watendaji) wa Serikali za Mitaa inatokana na ama Madiwani kuingilia kazi za utendaji au watendaji kuingilia kazi au majukumu ya kisiasa ya Madiwani.

Ili kuondoa tatizo hilo, Kanuni za Maadili ya Madiwani za mwaka 2000 zinaelekeza ifuatavyo:

(i) Kila Diwani na kila mtumishi wa Halmashauri, katika utekelezaji wa majukumu ya umma, atatakiwa kuwa na uhusiano mzuri utakaohakikisha ufanisi na utendaji bora wa kila upande.

(ii) Diwani aheshimiane na watumishi wa Halmashauri na aepuke kuwa na uhusiano wa karibu na mtumishi wa Halmashauri unaoweza kuathiri au kudhalilisha kila upande.

(iii) Diwani anakatazwa kuingilia shughuli za kiutendaji za Halmashauri kama vile:

  - Kutekeleza majukumu ya kitaaluma na kitaalam katika uendeshaji wa shughuli za Halmashauri;

  - Kutekeleza moja kwa moja maamuzi ya Halmashauri au sera za kitaifa.

(iv) Diwani au mtumishi wa Serikali za Mitaa, iwe ni kwa makusudi au uzembe anakatazwa kutoa taarifa za uongo au kutoa ushauri mbaya kwa Halmashauri. Iwapo Diwani au Afisa wa Halmashauri atavunja Kanuni hii (ya 28) na Halmashauri ikapata hasara, Diwani au afisa atawajibishwa

yeye mwenyewe au kwa pamoja kwa kulipa gharama ya hasara iliyopatikana. Hata hivyo, iwapo Diwani ametoa taarifa au ushauri kwa nia njema, hatawajibishwa. Kwa hiyo, kila Diwani na kila mtumishi hana uhuru bali anapaswa kutekeleza maagizo hayo ya sheria (Kanuni za Maadili ya Madiwani, 2000).

## 3. MWISHO

Maelezo yaliyotolewa hapo juu kwa ufupi yanatosha kuonesha kuwa Madiwani katika ujumla wao ndio mwajiri; na wao na watumishi wa Halmashauri kwa pamoja wanategemewa na wananchi na serikali wafanye kazi kama washiriki katika timu kwa maana ya kuendesha Halmashauri katika misingi iliyowekwa na sheria ili Halmashauri iweze kutoa huduma bora kwa wananchi wake. Kwa hiyo, ni muhimu sana pande zote mbili zishirikiane kwa sababu jukumu la kutoa huduma ni la wote ingawa kila mmoja ana eneo maalum analoshughulikia. Amani, kuaminiana na ushirikiano vikitawala, Halmashauri itaweza kupiga hatua nzuri ya maendeleo kuliko kupoteza muda mwingi katika mizozo.